

HEPATITIS C

Hepatitis C ni nini? (What is Hepatitis C?)

- Hepatitis maana yake ni uvimbeuchungu (maumivu na kuvimba) wa ini
- Hepatitis inaweza kusababishwa na kemikali, madawa, kunywa pombe kupita kiasi au virusi fulani
- Hepatitis C inasababishwa na virusi vya hepatitis C; kuna aina mbalimbali nyingi ya virusi hivi
- Karibia robo ya watu wanaoathirika watafuta virusi kutoka miili yao katika muda wa miezi sita
- Watu wengine wataendelea kuathirika na virusi kwa maisha mzima yao. Wengine wao watapata hasara ya ini au kansa ya ini baada ya miaka mingi.

Dalili za Hepatitis C ni nini? (What are the symptoms of Hepatitis C?)

Mara nyingi dalili hazionekani mpaka miaka mingi baada ya kuambukizwa virusi vya hepatitis C mwanzoni. Dalili zinaweza kuwa pamoja na:

- Uchovu
- Kupoteza hamu ya kula
- Kichefuchefu na kutapika
- Kuumwa chini ya ubavu upande wa kulia
- Homa
- Maumivu ya kia.
- Mabadiliko ya hali ya moyo na huzuni.

Hepatitis C inaeneza jinsi gani? (How is hepatitis C spread?)

Virusi vya hepatitis B vimo damu ya mtu aliyeathirika. Virusi vinaweza kuenezwa kwa njia ya:

- Vifaa vichafu vinavyotumiwa kwa kupiga sindano, kupasua, kung'oa meno, au kuchoma kwenye ngozi ya mwili kwa michoro
- Upaji wa damu unaoambukizwa. Damu inayotumika kwa upaji nchini Australia inapimwa kwa hepatitis C
- Kutumia vitu vya kibinafsi kama nyembe na miswaki (inayoweza kuwa na damu) vya mali ya mtu ambaye ana hepatitis C
- Wakati mwingine virusi vinaweza kueneza kwenda mtoto wa mwanamke aliye na hepatitis C wakati wa ujauzito au wa kuzaa. Hatari ni juu zaidi kama mama ameambukizwa karibu tu. Inaonekana hepatitis C haienezi kwa njia ya maziwa ya mama, ila kuna damu ndani maziwa
- Hepatitis C ina hatari kidogo sana kueneza kwa njia ya kujamiana, lakini inawezakana zaidi kidogo kama kuna mawasilano na damu.

Hepatitis C inatambuliwa jinsi gani? (How is hepatitis C diagnosed?)

- Kipimo cha damu kinaweza kuonyesha kama umeshawahi kuambukizwa na virusi vya hepatitis C. Inawezekana kuchukua hadi miezi 6 baada ya kuambukizwa mwanzoni mpaka kipimo cha damu kinaweza kugundua hepatitis C.
- Kipimo cha damu kinaweza kuonyesha pia kama umefuta virusi kutoka mwili wako.
- Kinga ya hepatitis B (kutoka protini inayopiga maambukizo) itakuwemo kwenye damu yako bado hata kama umeshafuta virusi
- Kama una kinga cha hepatitis C, na mwili wako haujafuta virusi, daktari yako anaweza kukuelekeza kwa daktari bingwa au zahanati maalum.

Hepatitis C inatibiwa jinsi gani? (How is hepatitis C treated?)

- Matibabu yanalenga kufuta hepatitis C kutoka mwili wako. Matibabu yanaendelea kwa muda ya miezi 6 hadi 12 na kwa kawaida yanapangaliwa na zahanati maalum ya ini.

Kama un hepatitis C utajisikia vizuri zaidi ukifanya hivyo:

- Acha kunywa pombe
- Kula chakula chenye lishe bora chenye mafuta kidogo
- Fanya mazoezi mara kwa mara
- Pumzika vizuri unapochoka.

Ni muhimu kumwona daktari yako kwa miadi ya mara kwa mara.

Je, ni lazima nimwambie yeyote kama nina hepatitis C? (Do I have to tell anyone if I have hepatitis C?)

Si lazima kumwambia yeyote kama una hepatitis C ila ukijitolea damu au ukiomba bima ya maisha.

Maelezo zaidi yanapatikana kwa (Further information is available from)